THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

NOVEMBER 1996

021 KISWAHILI

(Kwa Watahiniwa walioko na wasioko shuleni)

MUDA: Saa 3.00

---

MAAGIZO KWA MTAHINIWA

1. Jibu maswali manane (8) tu, maswali MANNE (4) kutoka Sehemu A na maswali YOTE ya Sehemu B.
2. Zingatia maagizo ya kila SEHEMU na ya kila swali.

Karatasi hii ina kurasa 5 zenye maandishi.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

## SEHEMU A: FASIHI

### Kifungu (i) Fasihi simulizi

(Jibu swali la 1 au la 2).

1. (a) Kwa kutumia mifano eleza njia tatu za kuhifadhi kazi za fasihi simulizi.

   (b) Eleza matatizo ya kila njia uliyoeleza.

2. Kwa kutumia mifano jadili umuhimu wa hadithi katika jamii.

### FASIHI ANDISHI

### Kifungu ii - Ushairi

| | |
|---|---|
| Mashairi ya Chekacheka | - T.A. Mvungi (ESC) |
| Mashairi ya Saadan | - S. Kandoro (Mwananchi P. LTD.) |
| Teuzi za Nafsi | - F. Semghanga (TUKI). |

3. Fafanua jinsi waandishi wawili kati ya hao waliotajwa wanavyosaidia kujenga jamii ya Tanzania.

4. Jadili matumizi ya lugha katika vitabu viwili kati ya hivyo vilivyotajwa.

### Riwaya (Hadithi)

| | |
|---|---|
| Kusadikika | - S. Robert (Nelson) |
| Shida | - N. Balisidya (DUP) |
| Kuli | - S.A. Shafi (TPH). |

5. Jadili masuluhisho yanayopendekezwa katika vitabu viwili kati ya hivyo vilivyotajwa ukionyesha kufaa au kutofaa kwake.

6. Eleza jinsi uumbaji wa wahusika ulivyofanikisha au kutofanikisha riwaya mbili kati ya hizo zilizotajwa.

### Tamthiliya

| | |
|---|---|
| Ngoswe | - E. Semzaba (ESC) |
| Harakati za Ukombozi | - P. Muhando (TPH) |
| Hawala ya Fedha | - A. Lihamba (TPH). |

7. Eleza umuhimu wa migogoro inayojadiliwa katika vitabu viwili kati ya hivyo vilivyotajwa hapo juu.

8. Chagua vitabu viwili kati ya vilivyotajwa. Kwa kila kitabu jadili dhima ya wahusika wawili katika kufikisha ujumbe.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

## SEHEMU B: LUGHA

Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuatia:

9. Ufahamu:

Aliacha shule akiwa darasa la kwanza, akawa mnyang'anyi, mvuta bangi na baadaye akatumikia kifungo cha miaka kumi jela. Baada ya adhabu hiyo, sasa ameamua kuwa mkulima. Huyo ni Sadiki Musa Mwangomba (34) mzaliwa wa Kyela mkoani Mbeya.

Ipo misemo mingi inayotoa maadili, maonyo na mafunzo kwa jamii kuhusiana na maisha ya kila siku, misemo ambayo mtu akiipuuza kuna uwezekano wa kupatwa na makuu. Miongoni mwa misemo hiyo ni Asiyesikia la mkuu huvunjika guu, Haraka haraka haina baraka, Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na dunia na mingi mingineyo. Bwana Sadiki anasimulia yaliyomsibu kuthibitisha ukweli wa misemo hii.

Bwana Sadiki alizaliwa mwaka 1961 katika kijiji cha Tenende wilayani Kyela na mwaka 1975 akaanza masomo ya darasa la kwanza katika Shule ya Msingi ya Tenende. Mwaka huo huo aliacha masomo hayo. Anasema sababu ya kuacha masomo ni kushawishiwa na vikundi mbalimbali vya kihuni. "Kwa sababu ya kutotumia vizuri ujana wangu, nilijiingiza katika vitendo ambavyo baadaye viliniletea matatizo makubwa hadi kunifanya nifungwe kwa muda wa miaka kumi". Alisema kwa kujutia.

"Nakumbuka nilipokuwa na wazazi wangu, matatizo mengi sana yalinipata kutokana na kunyanyaswa na baba yangu. Baadaye wazazi wangu walitengana, hali ambayo ilinilazimisha nikimbie nyumbani na kujiunga na vikundi vya kihuni. Hata hivyo ninamshukuru baba yangu, kwa kuwa alinifundisha kazi ya kilimo". Alibainisha Sadiki, akionesha amepania kulima kweli kweli.

Baada ya vitendo vyake vya kihuni kukithiri, na hasa baada ya kupatikana na hatia ya kuiba kwa kutumia nguvu, Sadiki alifikishwa mahakamani, ambako alitiwa hatiani kwa makosa ya uvutaji bangi, na unyang'anyi kwa kutumia nguvu. Hapo ndipo adhabu ya kifungo ilipomkabili. Huo ulikuwa mwaka 1983.

Baadhi ya magereza aliyopitia ni Luanda (Mbeya), Ukonga (Dar es Salaam), Maweni (Tanga) na mwisho ni Isanga (Dodoma).

"Nikiwa gereza la Maweni nilipata mateso makubwa sana kutokana na utetezi wangu wa haki zetu, sisi wafungwa dhidi ya askari jela. Harakati hizo zilinifanya nichomwe kwa moto mguu wangu wa kulia na maafande. Kitendo chao kiliniachia kovu kubwa hadi leo". Alisema huku akionesha kovu lake hilo kubwa...

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

"Na hapo ndipo nilipokumbuka mausia ya wazazi wangu waliyokuwa wakinipa kama vile, usiposikia la mkuu ulimwengu utakuhukumu, wewe ni mtoto wetu uliyezaliwa na sisi wenyewe lakini hutaki kutusikiliza, basi subiri uone dunia itakavyokueleza, alizidi kubainisha huku akionesha hali ya kujutia kwa kutozingatia maonyo hayo. Mwaka 1993 ndipo maisha ya jela yalipojitenga na kijana huyu, ambapo amedai baada ya hapo alikwenda moja kwa moja kijijini kwao Tenende. Huko alimkuta baba yake. Hata hivyo anasema alishindwa kuishi huko kutokana na matatizo makubwa aliyoyakuta huko.

Baadaye alimfuata mama yake anayeishi Bunda mkoani Mara. Alimkuta mama yake amezeeka. Hali hii ilimpa uchungu mkubwa sana, ambao anasema hatausahau.

"Kutokana na hali mbaya niliyomkuta nayo mama yangu, ndipo huruma iliponijia na hivyo nikaamua kuja Dar es Salaam kwa nia ya kuomba msaada wa hali na mali kutoka kwa mtu yeyote. Lengo langu ni kwamba niweze kujitegemea na baadaye niweze kuwasaidia wazazi wangu". Alizidi kuelezea malengo yake ya sasa.

Maswali:

(a) Kwa kutumia mifano eleza jinsi methali zilizopigiwa mistari katika aya ya pili zinavyohusiana na habari uliyosoma.

(b) Kwa nini Sadiki aliacha shule?

(c) Eleza mambo mabaya mawili ambayo wazazi wa Sadiki walifanya yaliyo-muathiri Sadiki maishani.

(d) Jambo gani zuri lilifanywa na wazazi wa Sadiki?

(e) Kwa maneno yasiyozidi ishirini eleza mafunzo aliyopata Sadiki gerezani.

(f) Andika kichwa cha habari hii kisichozidi maneno matano (5).

10. Andika insha yenye maneno yasiyozidi 200 kuhusu moja ya mada hizi:

(a) Mashindano ya urembo

(b) Uchaguzi Mkuu Tanzania

(c) Nikimaliza kidato cha nne ....

(d) Kuhifadhi wanyamapori.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

11. Eleza kwa mifano maana na kazi za:

    (a) kiambishi

    (b) mzizi

    (c) kihisishi

    (d) kiwakilishi.

12. Kwa kila sentensi zifuatazo onesha aina za vivumishi vilivyotumika:

    (a) Yule mrembo ameshika nafasi ya kwanza

    (b) Watu wangapi wana bendera nyekunde?

    (c) Mtoto mwenye baisikeli ana tabia nzuri

    (d) Meza yoyote itatufaa, mradi iwe nyororo

    (e) Hapa mjini magari madogo yanakwenda mbio sana.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner